



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



Machi 8,2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2023

Tarehe 8 Machi kila mwaka ni Siku ya Kimataifa ya kutambua utu, nafasi na mchango wa mwanamke katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa duniani. Umoja wa Mataifa uliridhia na kuanza kuadhimisha rasmi siku ya wanawake Duniani, Machi 8 mwaka 1975 kwa lengo la kuikumbusha dunia juu ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake. Uamuzi huu ulifikiwa ili kupinga mfumo dume ambao ulizikabili jamii mbalimbali duniani na kuminya haki za wanawake kama mionganini mwa makundi maalum.

Katika maadhimisho ya siku hii muhimu, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inaungana na jamii na wadau mbalimbali duniani kutambua mchango wa wanawake katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka 2023 ni "***Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia: Chachu Katika Kuleta Usawa wa Kijinsia.***" Kauli mbiu hii inatukumbusha kuona umuhimu wa ujumuishi wa wanawake katika

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Ploti Na. 201, Mtaa wa Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR
Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: info@chrugg.go.tz; zanzibar@chrugg.go.tz; Tovuti: www.chrugg.go.tz

masuala ya teknolojia na kutafakari juu ya namna teknolojia inavyoweza kuwa kichocheo au kizuizi cha kujiletea usawa wa kijinsia.

Kupitia kauli mbiu hii pia tunapata fursa ya kujadili na kuandaa mikakati madhubuti itakayosaidia kutumia teknolojia na kutatua changamoto zinazowakabili wanawake na makundi mengine yenye mahitaji maalum, zikiwemo zile zinazotokana na teknolojia yenyewe katika kutokomeza ukatili na kuleta usawa wa kijinsia.

THBUB inatambua kuwa teknolojia ikitumika vyema inakuwa chachu kwa maendeleo ya wanawake na Taifa kwa ujumla; Lakini ikitumika vibaya inaweza kuchangia uvunjifu wa haki za binadamu. Katika kipindi hiki cha maendeleo ya teknolojia duniani, kumekuwepo na changamoto za matumizi ya teknolojia ambapo wakati mwingine imechangia ukatili wa kijinsia. Mathalani, baadhi ya watu, hasa wapenzi kutumia simu na vifaa vingine vya kielektroniki kujirekodi wakiwa katika faragha lakini pale inapotokea kutolewana picha hizo zimekuwa zikirushwa mitandaoni kwa lengo la kudhalilisha ambapo wahanga wengi wa matukio haya wamekuwa ni wanawake na watoto. Aidha, kumekuwepo maendeleo hafifu ya matumizi ya teknolojia katika maeneo ya vijiji tofauti na mijini.

Kwa kuzingatia kauli mbiu ya mwaka huu, Tume:

- i) Inaihamasisha jamii kuendelea kutumia teknolojia kwa weledi, kwa kuzingatia sheria, haki za binadamu na misingi ya utawala bora.
- ii) Inatoa wito kwa wanawake kuendelea kujiamini na kutumia teknolojia katika kujiletea maendeleo yao kiuchumi na kijamii; na

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Ploti Na. 201, Mtaa wa Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: info@chragg.go.tz, zanzibar@chragg.go.tz; Tovuti: www.chragg.go.tz

- iii) Inaiomba Serikali na wadau mbalimbali kuandaa programu maalum kuwasaidia wanawake hasa wa vijijini kutumia teknolojia katika kujikwamua kiuchumi na kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Imetolewa na:



Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)

Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Machi 8, 2023

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Ploti Na. 201, Mtaa wa Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR
Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)
Barua Pepe: info@chragg.go.tz, zanzibar@chragg.go.tz; Tovuti: www.chragg.go.tz